

JINA:.....NAMBARI:.....

SHULE:.....SAHIHI:.....

TAREHE:.....

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

JULAI/ AGOSTI 2014

MUDA: Saa 2  $\frac{1}{2}$

## MITIANI WA PAMOJA WA WILAYA YA KISII KUSINI-2014.

*Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)*

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

JULAI/ AGOSTI 2014

MUDA: Saa 2  $\frac{1}{2}$

### **MAAGIZO:**

- a) Jibu maswali **manne** pekee.
- b) Swalii la **kwanza** ni **LAZIMA**.
- c) Chagua maswali mengine **matatu** kutoka sehemu **nne** zilizobaki yaani, Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi simulizi.
- d) Usijibu maswali kutoka sehemu moja.
- e) Kila swali lina alama 20

*Hii karatasi ina kurasa 4 zilizopigwa chapa.*

*Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote mbili za karatasi hii ya mtahini zimepigwachapa sawasawa  
Na kuwa maswali yote yamo.*

**SWALI LA LAZIMA: SEHEMU YA A: HADITHI FUPU.  
DAMU NYEUSI.**

1. Eleza masaibu ya fikirini kule ughabuni ukirejelea hadithi ya damu nyeusi. Al.20

**SEHEMU YA B. RIWAYA: Kidagaa kimemwozea.**

2. Jadili maudhui haya;  
i) Uongozi mbaya. Al.10  
ii) Utabaka. Al. 10
3. Eleza matumizi ya mbinu kinaya katika riway hii al.20.

**SEHEMU YA C: TAMTHILIA : MSTAHIKI MEYA.**

4. “Siha pingamizi kwa maana hii ni grand idea.”  
a) Nani anayesema maneno haya. al.2  
b) Eleza muktadha wa dondo hii. al .4  
c) Chambua sifa za mhusika anayesema maneno haya. al.4  
d) Taja waliokua pamoja na mnenaji katika kadhia hii. al.3  
e) Toa mbinu iliyotumika katika dondo hii al.1
5. Nchi za kiafrika zinakumbwa na changamoto tele thibitisha kauli hii ukizingatia tamthilia ya mstahiki meya al 20

**6. SEHEMU YA D: USHAIRI.**

Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali yafuatayo;

Yamerundikwa machicha, na maganda ya matunda,  
Na mwiko uliochacha, na mbali uliovunda,  
Harufu inaposecha, yanukia naipenda,  
Hakuna inamchusha, bustani ya maua.

Mianzi yetu ya pua, imeota pasigaa,  
Hasia zinobagua, mara mbili zinafaa,  
Kibaya tunarudua, kizuri kina balaa,  
Tope ziwe ni halua, na samli imekaa.

Macho yameota kungu, ilaa yaona yote,  
Hata likitanda wingu, anga litatanda kote,  
Ni mzuri ulimwengu, wa furaha na wa kite,  
Na bustani mwenzangu, kipita siteme mate.

Mahame na maanguko, machoni yanapumbaza,  
Kifusi na mafuniko, moyoi yanaliwaza,  
Mapakacha ya rundiko, topasi yanampozza,  
Hakuna inomchusha, bustani ya maua.

Kuku anapara kucha, na bata tope aponda,  
Mbwa pua inapucha, pipani anamowinda,  
Taka zimejenga picha, inovutia kushinda,  
Vitalu vyenye mahaba, ni lazima kuvilinda.

Mbu wanazaliana, mbu wajidunduliza,  
Njiani tunapishna, nzi wanatubuiza,  
Maradhi huzidiana, twacheka tukipuuza,  
Liwazo kubwa si haba bustani yapendeza.

**Maswali.**

- a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (alama 2)
- b) Shairi hili ni la aina gain? Toa sababu mbili. (alama 2.)
- c) Eleza vitu vitatu vya kuchukiza ambavyo amevizungumzia mshairi. (alama 3)
- d) Eleza ujumbe wa mtunzi kuhusu mabustani ya vitalu vya maua. (alama 4.)
- e) Eleza umbo la shairi hili. (alama 5.)
- f) Kwa nini mshairi anasema kuwa macho yameota kungu katika ubeti wa tatu? (alama 2)

**7. SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

- a) Eleza maana methali. al.2
- b) Taja sifa tano za methali. al.5
- c) Toa umuhimu wa methali za fasihi simulizi. al.5
- d) Eleza matumizi ya methali za fasihi simulizi katika jamii. al.8